KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 12, Issue 4

21st SHA'BAAN 1432

22nd July, 2011

YALIYOMO

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUM[Prt.2] 1 - 4

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUMU [Pt. 2]

Na: Sheikh Muhammad Saalih Al-Munajjid

HUTAMBULIWAJE IINGIAPO RAMADHAAN.

(9) Kuingia kwa Ramadhaan huthibitishwa kwa kuonekana mwezi kongo, au kwa kukamilisha siku thalathini za Sha'baan. Yoyote atakaeuona mwezi kongo au atakaeusikia kutoka kwenye asili yenye kuaminika atawajibika kufunga. Utumiaji wa hesabu za kupanga katika kutambua kuingia kwa Ramadhaan ni bid'ah, kwa sababu hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) imeeleza waziwazi yakwamba: "Fungeni muuonapo (mwezi kongo) na mufungue saumu zenu muuonapo." Iwapo Muislamu mtu mzima, mwenye akili timamu, muaminifu na anaetegemewa akiwa na uwezo wa kuona kwa macho atasema yakwamba ameuona kwa macho yake, basi tutayachukuwa neon lake kwa hilo na tuwajibike kulingana na hali ilivyo (yaani; tuanze kufunga).

NI NANI ANAEWAJIBIKA KUFUNGA?

(10) Kufunga ni wajibu wa kila Muislamu mtu mzima, mwenye akili timamu, na aliye mkaazi (yaani; asiyekuwa msafiri) aliye na uwezo wa kufunga na akawa hana kitu mfano wa haidh (damu ya ada ya mwanamke ya kila mwezi) au nifaas (damu ya mazazi) itakayomzuiya asiweze kufunga. Mtu aliyefikiya umri wa kubaleghe na akatokewa na chochote miongoni mwa mambo matatu: kutokwa na manii, emma kwenye ndoto au isiyokuwa hivyo, kuota kwa nywele zinazokwaruza kwenye sehemu zake za siri; kufika umri wa miaka kumi na tano. Katika hali za wasichana, kuna jambo la nne liitwalo kuingia mwezini; msichana anapovunja ungo (anapoingia mwezini kwa mara ya kwanza), atawajibika kufunga hata kama hajafika umri wa miaka kumi.

(11) Vijana wanatakiwa waamrishwe kufunga wafikapo umri wa miaka saba, iwapo wataweza kufanya hivyo, na baadhi ya wanavyuoni wamesema yakwamba motto na achapwe afikapo umri wa miaka kumi iwapo hatofunga, kama ilivyo katika hali ya swala (Angalia katika al-Mughnee, 3/90). Mtoto hupewa zawadi kwa kufunga, na wazazi wakalipwa malipo mema kwa kumlea vyema mtoto na kumuongoza kwenye njia nzuri Al-Rubay' bint Mu'awwidh (رضي الله عنها) amesema katika kuzungumzia kuhusu Ramadhaan ilipofanywa kuwa ni waajib: "Tulikuwa tukiwafanya watoto wetu wafunge, na tukawa tunawatengezea sanamu kutokamana na manyoya. Atakapokuwa mmoja

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

JIPATIE KITABU CHA

"SAUMU YA MWEZI WA RAMADHAAN KAMA ILIVYOTEKELEZWA NA MTUME (صلى الله عليه وسلم)."

TUPIGIE SIMU KATIKA NAMBA HIZI:

+254- 0721473181 AU

+254-0727341779



TANGAZO LA DARSA ZA RAMADHAAN 2011/1432H

MASJID MAZRUI [KILA SIKU BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMATATU HADI JUMATANO / [Nawaaqidh ul-Islaam] / Ustadh Athman Bin Na'man

ALKHAMIS / [-] / Ustadh Sharrif

JUMAMOSI NA JUMAPILI / [AL-WAABIL AS-SWAYYIB] / Abu 'Abdur-Razzaq Haruna Rass.

MASJID KHAYRAAT [KIZIWI] [BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMANNE NA ALKHAMIS / [Ustaadh Muhammad Abdillah]

JUMATANO / [TAS-HEEL AL-AQEEDAH] / Abu 'Abdur-Razzaq Haruna Rass.

Unaweza kusikiliza Darsa hizi kwenye Mtandao (Internet)

Pal-Talk ⟹ All-Rooms ⟹ Religion & Spirituality ⟹ Callers to Tawheed ⟹ Swahili Duroos.

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

wao analia kwa ajili ya njaa, ndipo tulipokuwa tukimpa sanamu huyo acheze nae mpaka ifikapo wakati wa kufungua saumu zao." (al-Bukhaari, Fath, no. 1960). Baadhi ya watu hudhania yakwamba si muhimu kwao kuwahimiza watoto wao wafunge; kwa hakika, mtoto huwenda akawa na shauku kubwa kuhusu kufunga na akawa na uwezo wa kufanya hivyo, lakini huwenda babake au mamake akamkataza kufunga, kutokamana na chembelecho wasemavyo, "twamsikitikiya". Hawazingatii wao yakwamba masikitiko ya kweli na huruma ni inahusika ndani yake na kumzoezesha kufunga. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) [tafsiri ya maana]: **"Enyi Mlioamini! Jiokoeni nafsi zenu na watu wenu, na moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanusimamia Malaika wakali wenye nguvu, hawamu'asi Allaah kwa amri Zake; na wanatenda wanayoamrishwa (yote)."** [al-Tahreem 66:6]. Ni lazima tahadhari ya ziyada iangaziwe katika suala la saumu ya msichana pindi aingiapo kwenye umri wa kubaleghe, kwa sababu anaweza kufunga pindi aingiapo kwenye ada yake, kutokana na kuona haya, na baadae asilipe siku anazodaiwa.

(12) Iwapo kafiri atasilimu, au mtoto atakapofika umri wa kubaleghe, au mwenda wazimu atakapozindukana katika wakati wa mchana, watahitajika kujiepusha na kula kwa siku nzima iliyobaki, kwa sababu wao watakuwa ni miongoni mwa wenye kuwajibika kufunga, lakini hawawajibiki kuzilipa siku za Ramadhaan ambazo walizozikosa, kwa sababu katika wakati huo hawakuwa ni miongoni mwa waliowajibika kufunga.

(13) Wendawazimu hawana jukumu kwa matendo yao (matendo yao hayahifadhiwi), lakini iwapo mtu atakuwa na wazimu mara nyengine na mara nyengine akawa mzima, ni lazima afunge katika nyakati zake anapokuwa mzima. Ikiwa atashikwa na wazimu katika wakati wa mchana, hilo halitaharibu saumu yake, kama ambavyo ilivyo iwapo mtu atazimia kutokana na ugonjwa au sababu nyengine, kwa sababu alikuwa na niya ya kufunga alipokuwa na akili yake timamu.(Majaalis Shahr Ramadhaan cha Ibn 'Uthaymeen, Uk.28). Hukmu kama hiyo inafanana na suala la ugonjwa wa kifafa.

(14) Iwapo mtu atakufa katika wakati wa Ramadhaan, atakuwa hana "Deni" juu yake au warathi wake kuhusiana na masiku yaliyobaki ya mwezi.

(15) Ikiwa mtu alikuwa hajui yakwamba kufunga katika mwezi wa Ramadhaan ni faradhi, au yakwamba ni haraam kula au kuingiliana kimapenzi baina ya mume na mkewe katikia mchana wa mwezi huu, basi kulingana na Jamuhuri ya wanavyuoni, sababu hii inakubalika, kama vilevile ilivyo kumuhusu mtu aliyeanza kusilimu, Muislamu anayeishi kwenye Daar al-Harb (nchi za Makafiri) na Muislamu aliyekulia miongoni mwa Makafiri. Lakini mtu aliyekulia miongoni mwa Waislamu na akaweza kuuliza masuali na kujionea mwenyewe, hatokuwa na sababu.

WASAFIRI

(16) Kwa msafiri kuruhusiwa kuwacha kufunga, ni lazima masharuti Fulani yapatikane. Safari yake itatakikaniwa kuwa na masafa marefu, laa si hivyo, basi angalau ijulikane yakwamba ni mwenye kusafiri (ingawaje kuna ikhtilafu maarufu sana miongoni mwa wanavyuoni kuhusu suala hili), na afike nje ya Mji na vitongoji vyake. (Wanavyuoni wengi wanasema yakwamba hafungui saumu yake kabla hajapita mipaka ya Mjini). Wanasema yakwamba kihakika safari haijaanza mpaka mtu avuke mipaka ya Mji, na mtu ambaye bado yuko kwenye Mji huwa ni "mkaazi" na "yupo". Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) [tafsiri ya maana]: **"kwahivyo, atakaeuona (mwezi kongo katika usiku wa kwanza wa) mwezi (wa Ramadhaan; yaani atakaekuwa nyumbani kwake) atalazimika kufunga ..."** [al-Baqarah 2:185]. Huwa hahesabiki kama msafiri mpaka atoke nje ya Mji; na iwapo bado atakuwa ndani ya Mji; atatambulika kama mtu aliye nyumbani, kwahiyo haruhusiwi kufupisha swala zake. Vilevile safari yake isiwe ni safari yenye malengo ya ufisadi na uchafu (kulingana na wanavyuoni wengi), au kwa malengo ya kujaribu kusafiri ili apate fursa ya kutofunga.

(17) Msafiri anaruhusiwa kuwacha kufunga, kulingana na maafikiano ya Umma, iwapo atakuwa na uwezo wa kuendelea kufunga au hatokuwa na uwezo, na iwapo itakuwa ni vigumu kwake kufunga au laa. Hata kama safari yake ni ya urahisi na akawa na mtu wa kumuhudumikia, bado ataruhusiwa kufungua saumu yake na kufupisha swala zake (Majmoo' al-Fataawaa, 25/210).

(18) Yoyote mwenye kuazimia kusafiri katika mwezi wa Ramadhaan hafai kuwa na niya ya kufungua saumu yake mpaka awe ameianza safari yenyewe, kwa sababu huwenda kukatokea kitu kikamzuiya asiweze kuianza safari yake (Tafseer al-Qurtubi, 2/278). Msafiri hafai kuvunja saumu yake mpaka azivuke nyumba wanazoishi watu wa mjini mwake; akisha kuvuka mipaka ya mjini, ataweza kufungua saumu yake. Vilevile, iwapo ataruka kwa Ndege, pindi Ndege itakapokuwa imeshaondoka na kuvuka mipaka ya mjini, anaweza kufungua saumu yake. Iwapo Uwanja wa Ndege utakuwa nje ya Mji wake, anaweza kufungua saumu yake hapo, lakini iwapo uwanja wa Ndege utakuwa ndani ya Mji wake au imeshikana na mji, hatofungua saumu yake katika uwanja wa Ndege kwa sababu yeye bado atakuwa angali ndani ya mji wake.

(19) Jua likitwa na akafungua saumu yake akiwa kwenye ardhi, kisha Ndege ikapaa (ikaondoka), mara akaliona jua, ataendelea kula kwa sababu atakuwa ameshakamilisha saumu ya siku, na haiwezekani kurudia kitendo cha 'Ibada iliyomalizika. Ikiwa Ndege imepaa kabla ya kutwa kwa jua na akawa anataka kuikamilisha saumu ya siku hiyo katika safari yake, asifungue saumu yake mpaka jua litwe kutoka mahali popote atakapokuwa angani. Rubani haruhusiwi kuishusha Ndege chini katika ALTITUDE kutoka mahali ambapo jua lisipoweza kuonekana kwa min-ajil ya malengo ya kufungua saumu, kwa sababu hii itakuwa ni miongoni mwa sampuli ya ujanja, lakini iwapo ataishusha Ndege chini kwa sababu zenye kueleweka, na ikawa matokea yake mkate wa jua ukapotea, basi ataruhusiwa kufungua saumu yake (Kutoka katika fataawa za Shaykh Ibn Baaz, zilizotolewa kwa njia ya mazungumzo).

(20) Yoyote mwenye kusafiri na kwenda mahali na akakusudia kukaa hapo kwa zaidi ya siku nne atalazimika kufunga, kulingana na

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

wanavyuoni wengi. Kwahivyo, iwapo mtu atasafiri kwenda kusoma katika nchi ya ng'ambo kwa muda wa miezi au miyaka, basi hapo kulingana na wanavyuoni wengi - wakiwemo ma-Imaam wane - atazingatiwa kuwa ni miongoni mwa "wakaazi" hapo na kwahiyo atawajibika kufunga na kuswali swala zake kwa ukamilifu. Ikiwa msafiri atapita kwenye mji usiokuwa wake, hatokuwa na haja ya kufunga, mpaka ikiwa kukaa mahali hapo itakuwa ni zaidi ya siku nne, ambapo katika hali kama hiyo itamlazimu kufunga, kwa sababu hukmu inayowahusu wenye "kuishi" vilevile zitamuhusu yeye. (Angalia katika Fataawa al-Da'wah cha Ibn Baaz, 977).

(21) Yoyote mwenye kuanza kufunga akiwa katika hali ya "utulivu" huanza kufunga haliyakuwa ni "mkaazi" kasha akaanza safari katika mchana anaruhusiwa kufungua saumu yake, kwa sababu Allaah amefanya kuondoka kwa ujumla kuwa ni sababu ya kisheriya ya kutofunga. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) [tafsiri ya maana]: **"... na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi (atimize) hisabu (ya siku alizowacha kufunga) katika siku nyingine ..."** [al-Baqarah 2:185]

(22) Mtu mwenye kawaida ya kusafiri anaruhusiwa kutofunga iwapo atakuwa na nyumba atakayokuwa akiirudia, kama vile mjumbe mwenye kusafiri kwa ajili ya kuhudumikia shughuli za Waislamu (na pia madereva wa gari za abiriya, marubani, na wafanyi kazi wa mashirika ya Ndege, hata kama usafiri wao ni wa kila siku - lakini itawabidi kuzilipa baadae siku watakazokosa kufunga). Hayo pia yatawahusu mabaharia wenye nyumba katika nchi-kavu, lakini iwapo baharia atakuwa na mkewe na mahitaji yake yote ndani ya Meli, na akawa ni mwenye kusafiri mara kwa mara, basi hatoruhusiwa kufungua saumu yake wala kufupisha swala zake. Ikiwa mabedui wenye kuhama kutoka kwenye nyumba zao za Baridi hadi kwenye nyumba zao za joto, au kinyume chake, wataruhusiwa kufungua saumu zao na kufupisha swala zao, lakini mara tu watakapotulizana emma kwenye nyumba zao za Baridi au Joto, hawafai kufungua saumu zao wala kufupisha swala zao, hata kama watakuwa wakiwafuata mifugo yao. (Angalia kwenye Majmoo' Fataawa Ibn Taymiyah, 25/213).

(23) Iwapo Msafiri atawasili katika wakati wa mchana, kuna mabishano maarufu mno miongoni mwa wanavyuoni kuhusiana na iwapo atajizuiya kula na kunywa (Majmoo' al-Fataawa, 25/212). Lakini, kwa kuchukuwa msimamo wa hadhari, ni bora ajizuiye na kula na kunywa, kutokana na kuuheshimu mwezi huu, lakini itamlazimu ailipe siku hiyo baadae, emma iwapo alijizuiya kula na kunywa baada ya kuwasili kwake.

(24) Ikiwa aliianza Ramadhaan katika Mji mmoja, kasha akasafiri kuelekea kwenye Mji mwengine ambapo watu walianza kufunga kabla yake au baada yake, hapo itambidi afuate hukmu inayowahusu watu wa Mji alikokwenda, kwahivyo atamalizia Ramadhaan pindi watakapomaliza Ramadhaan, hata kama itamaanisha yakwamba atafunga zaidi ya siku thalathini, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Fungeni iwapo kila mmoja atafunga, na mufunguwe saumu zenu iwapo kila mmoja atafunguwa saumu yake."* Ikiwa itamaanisha yakwamba saumu yake itakuwa ni pungufu kuliko siku ishirini na tisa, itamlazimu kulipa baada ya 'Eid, kwa sababu mwezi wa Hijri hauwezi kuwa chini ya siku ishirini na tisa. (Kutoka katika Fataawa al-Shaykh 'Abd al'Azeez ibn Baaz: Fataawa al Siyaam, Daar al-Watan, Uk. 15-16)

WAGONJWA

(25) Yatokeapo maradhi ambayo yenye kuwafanya watu wakawa wagonjwa, mtu ataruhusiwa kuwacha kufunga. Msingi wa haya ni aya aliposema Allaah (سبحانه وتعالى) [tafsiri ya maana]: **"... na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi (atimize) hisabu (ya siku alizowacha kufunga) katika siku nyingine ..."** [al-Baqarah 2:185]. Lakini iwapo maradhi yenyewe ni madogo, kama kikohozi au kuumwa na kichwa, basi hiyo haitokuwa ni sababu ya mtu kufungua saumu yake. Ikiwa kutakuwa na ushahidi wa matibabu, au mtu akawa anajijua kutokana na uzoefu wa hali yake, au atakuwa na uhakika, yakwamba kufunga kutaleta madhara katika afya yake au kutachelewesha kupona kwake, ataruhusiwa kufunguwa saumu yake; kwa hakika itakuwa ni makuruhu kwake kufunga kwenye hali kama hiyo. Iwapo mtu atakuwa na maradhi ya hatari, hatokuwa na haja ya kuwa na niya katika wakati wa usiku ya kufunga kesho, hata kama kuna uwezekano yakwamba huwenda kukipambazuka akawa ni mzima, kwa sababu linalohisabika ni wakati ule alivyo.

(26) Iwapo kufunga kutasababisha kupotewa na fahamu, itambidi afunguwe na ailipe siku hiyo baadae (al Fataawa, 25/217). Mtu akipotewa na fahamu katika wakati wa mchana na akazindukana kabla ya Maghrib au baada yake, saumu yake itakuwa haina mushkili, maadamu alikuwa amefunga katika wakati wa asubuhi; ikiwa alipotewa na fahamu kuanzia alfajiri mpaka Maghrib, basi kulingana na wanavyuoni wengi ni kwamba saumu yake haifai. Kulingana na wanavyuoni wengi, ni wajibu wa mwenye kufunga atakaepotewa na fahamu zake alipe saumu zake baadae, bila ya kujali ni kwa wakati gani alipotewa na fahamu. (Al-Mughni ma'a al-Sharh al-Kabeer, 1/412, 3/32; al-Mawsoo'ah al-Fiqhiyyah al-Kuwaytiyyah, 5/268). Baadhi ya wanavyuoni hutoa fatwaa kiasi cha kwamba mtu mwenye kupotewa na fahamu au akachukuwa tembe za usingizi au akadungwa sindano za ganzi kwa sababu ifaayo, na akapotewa na fahamu kwa siku tatu au chache, itamlazimu alipe siku hizo baadae, kwa sababu atazingatiwa kuwa kama mwenye kulala; iwapo atapotewa na fahamu kwa zaidi ya siku tatu, hatokuwa na haja ya kuzilipa siku hizo kwa sababu atazingatiwa kuwa ni kama mtu mwenda -wazimu. (Kutoka kwenye fataawa za Shaykh 'Abd al- Azeez ibn Baaz, alizozitoa kwa kauli yake).

(27) Iwapo mtu atashikwa na njaa ya ajabu au kiu, mpaka akahofiya yakwamba huwenda akafa, au yakwamba baadhi ya sehemu za kiwiliwili chake huwenda ikawa zimeharibika na haziwezi kurekebishika, na akawa na sababu za kimsingi za kuamini hivyo ilivyo, anaweza kufungua saumu yake na ailipe katika siku za baadae, kwa sababu kujiokoa maisha yako ni waajib. Lakini hairuhusiwi kufungua saumu kwa sababu ya matatizo Fulani yawezayo kukabiliwa au kiwa sababu mtu amechoka au alikuwa

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

akiwaza na kuhofia aina fulani ya maradhi. Watu wenye kufanya kazi kwenye sehemu za dharubu yenye kuumiza hawaruhusiwi kufungua saumu zao, na inawalazimu kuwa na niya tangu usiku ya kufunga siku ifuatayo. Ikiwa hawawezi kuwacha kazi na wakawa wanahofia yakwamba huwenda wakapata madhara fulani, katika wakati wa mchana, au wakapambana na dharubu nzito sana zilizowasababisha wao kufungua saumu zao, basi na wale kiasi kitakachowawezesha tu kuhimili kulemewa kwao na janga hilo, kisha na wajizuiye na kula (wasile tena) mpaka jua litwe, na itawabidi wailipe siku hiyo baadae. Wafanyi kazi kwenye mashirika ya kazi za dharubu, kama vile kazi za tanuu la Joto na kuyeyusha vyuma, wangejaribu kubadilisha masaa yao ya kazi ili wapate kufanya kazi wakati wa usiku, au wachukuwe mapumziko yao katika wakati wa Ramadhaan, au hata wachukuwe mapumziko yasiyokuwa ya malipo, lakini iwapo hayo hayatokuwa na uwezekano, basi na wajitafutie kazi nyengine ambapo watakapoweza kujumuisha majukumu yao ya ki-Dini na ki-Duniya: **"… Na anayemuogopa Allaah, (Allaah) humtengenezea njia ya kuokoka (katika kila balaa). Na humpa riziki kwa namna asiyoitazamia, (asipopatazamia) …"**[al-Talaaq 65:2-3 – maana ya tafsiri]. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/233, 235). Mitihani ya wanafunzi sio sababu ya mtu kufungua saumu yake katika wakati wa Ramadhaan, na hairuhusiwi kuwatwi'i wazazi katika kufungua saumu kwa ajili ya kufanya mitihani, kwa sababu hakuna utwi'ifu kwa kiumbe chochote iwapo kutahusika ma'asiya kwa Muumba (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/241).

(28) Mgonjwa mwenye matumaini ya kupoa asubiri mpaka apate afuweni, kisha na azilipe saumu alizozikosa; haruhusiwi kuwalisha masikini tu. Mgonjwa wa maradhi ya kudumu na akawa hana matumaini ya kutibika na wazee wakongwe wasioweza kufunga na wamlishe masikini kwa nusu Saa' ya chakula cha kawaida cha Nchini mwake kwa kila siku aliyoiwacha kuifunga (Nusu Saa' ni takriban Kilo Moja Na Nusu ya Mchele). Inaruhusiwa kwake kufanya hivyo kwa pamoja, katika siku moja mwishoni mwa mwezi, au amlishe masikini mmoja kwa kila siku. Na afanye hivi kwa kutoa chakula chenyewe, kwa sababu ya matamshi ya aya - hawezi kufanya hivyo kwa kuwapa masikini pesa (Fataawa al-Lajnah al- Daa'imah, 10/198). Lakini anaweza kumpa pesa mtu muaminifu au Chama Cha Kutoa Msaada wakanunue chakula na wawagawanyie masikini kwa niyaba yake. Ikiwa mgonjwa hafungi katika mwezi wa Ramadhaan, akisubiri kupoa ili apate kuzilipa siku baadae, kisha akagundua yakwamba maradhi yake ni ya kudumu, itamlazimu kumlisha msikini kwa kila siku ambayo hakuifunga. (Kutoka katika fataawa za Shaykh Ibn 'Uthaymeen). Ikiwa mtu anasubiri kupoa kutoka kwenye maradhi na anatarajia kupata afuweni, lakini mara akafa, hatokuwa na "Deni" analodaiwa wala warathi wake. Iwapo maradhi ya mtu yatazingatiwa kuwa ni ya kudumu, basi hatofunga na badala yake atawalisha masikini, kisha ajiendeleze kwenye utabibu zaidi kumaanisha yakwamba sasa amepata utabibu anaoutumia na kuweza kumponya, hatowajibika kuzilipa siku alizokuwa akidaiwa, kwa sababu ametekeleza aliyowajibika kuyafanya katika wakati wa kuwajibika. (Fataawa al-Lajnah al Daa'imah, 10/195)

(29) Iwapo mtu ni mgonjwa, kisha akapoa, na akawa ajiweza kulipa siku zake anazodaiwa lakini asizilipe mpaka akafa, basi zitachukuliwa pesa kutoka katika hazina yake za kumlisha masikini kwa kila siku aliyoikosa. Ikiwa yoyote miongoni mwa jamii yake wakitaka kumfungia kwa niyaba yake, basi hii INAJUZU, kwa sababu imepokewa katika swaheehayn yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Yoyote atakaekufa haliyakuwa anadaiwa saumu, warathi wake na wamfungie kwa niyaba yake.*" (Kutoka katika Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, volume kuhusu Da'wah, 806).

WATU WAZIMA [WAKONGWE]

(30) Watu wazima (wakongwe) ambao waliopoteza nguvu zao na ambao wanaendelea kudhoofika kila kukicha yakiwa mauti yanawasongelea, hawana haja ya kufunga, na wanaruhusiwa wasifunge maadamu kufunga itakuwa ni jambo gumu kwao. Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) alikuwa akisema kuhusiana na aya [tafsiri ya maana]: **"Na kwa wale wanaofunga kwa mashaka (k.m; mtu mzima), wao wanakhiyari ya kuchagua (emma wafunge au) kumlisha masikini (kwa kila siku moja)."** [al Baqarah 2:184]: "Hukmu hii haikufutwa. Inamuhusu mtu mzima - mume na mtu mzima - mke, ambao wasioweza kufunga, kwahiyo na wawalishe masikini kwa kila siku moja." (Al-Bukhaari, Kitaab al-Tafseer, Baab Ayaaman Ma'doodaat…) Na wale waliodhoofika na kuchanganyikiwa hawana haja ya kufanya kitu chochote chengine, na jamii zao pia hawana haja ya kuwafanyia chochote kwa niyaba yao, kwa sababu watu kama hao hawajiwezi tena kupambana na majukumu. Iwapo fahamu zao zitakuwa njema katika wakati fulani na wakati mwengine hazijifai, itawabidi wafunge pindi wanapokuwa ni WAZIMA na hawana haja ya kufunga wanapokuwa si wazima. (Angalia katika Majaalis Shahr Ramadaan cha Ibn 'Uthyameen, Uk. 28).

(31) Kwa wale wenye kupigana vita na maadui au waliozingirwa na maadui, iwapo kufunga kutazidi kutawadhoofisha wasiweze kupigana, wataruhusiwa kufungua saumu zao, hata kama wao si wasafiri. Wakihitaji kufungua saumu zao kabla ya vita, wanaweza kufungua saumu zao. Siku moja Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaambia Maswahaba zake kabla hwajaanza kupigana: *"Kukipambazuka mutakutana na maadui zenu na kutofunga kutawapa nguvu, kwahivyo musifunge."* (Imepokewa na Muslim, 1120, 'Abd al-Baaqi edn. Hii pia ndiyo rai aliyoipendekeza Shaykh al-Islam Ibn Taymiyah. Wanavyuoni wa Damascus vilevile walitoa fatwa zao kwenye mas'ala hayo wakati Mji wao ulipovamiwa na kina Tartar)

(32) Iwapo sababu ya mtu ya kutofunga iko wazi, kama vile maradhi, hapatokuwa na makosa yoyote akila na kunywa waziwazi, lakini iwapo sababu itafichikana, kama vile ada ya mwezi ya mwanamke, ni bora kwake kula na kunywa kwa siri, ili asije akavutia tuhuma na mfano wake.

NENO LA BUSARA

"HAKUNA KHERI KATIKA URAFIKI KWA YULE ASIYEONA KWAKO KHERI KULIKO NAFSI YAKE."